
# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA MNISPAA YA KIGAMBONI

## MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:
## TUMESHIKAMANA NA TUMAENDELEO YA TAIFA LETUMEIMARIKA KWA

***Toleo Maalum la Miaka 60 ya Muungano***












# DUA NA SALA YA KULIOMBEA TAIFA




Mkuu wa Wilaya akiliombea Taifa katika Dua Maalum ya kuliombea Taifa

Katika kuelekea Maadhimisho ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni Mhe. Halima Bulembo aliongoza Dua maalum ya kuliombea Taifa iliyofanyika katika Ukumbi wa chuo cha Maeendeleo ya Wananchi Wilayani hapo.



Kiongozi wa Dini ya Kiislamu akiongoza Sala ya kuliombea Taifa

Katika Dua hiyo D.C  Bulembo aliwataka Wananchi wa Kigamboni kuuenzi Muungano ulioanzishwa na waasisis muhimu wa Taifa hili akiwemo Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere,  pamoja na Hayati Abeid Aman Karume.



Mchungaji Toka Dini ya Kikristo akiongoza sala

Akielezea mafanikio Wilayani humo DC amesema katika miaka 60 ya Muungano Wilaya ya Kigamboni imepiga hatua kubwa katika utoaji wa huduma za kijamii ikiwemo Elimu, Afya, Maji pamoja na Barabara

Aidha alisema Wilaya imefanikiwa kujenga shule 35 za Serikali wilayani humo na kwa upande wa Sekta ya Afya Wilaya imefanikiwa kujenga vituo vya Afya vipatavyo 27 ambapo kwa namna moja au nyingine viimesogeza huduma muhimu kwa Wananchi.

# MICHEZO



Baadhi ya wachezaji wa

Wilaya ya Kigamboni iliweza kuendesha Bonanza Maalumu ambalo lilihusisha michuano mbalimbali ikiwemo shindano la Insha lililohusisha Wanafunzi kutoka katika shule mbalimbali Wilayani humo

Pia ilifanyika michuano ya mchezo wa mpira wa Miguu uliohusisha Timu mbaalimbali Wilayani humo

Pia ilifanyika michuano ya mchezo wa mpira wa Miguu uliohusisha Timu mbalimbali Wilayani humo

Akiongoza zoezi la ugawaji wa zawadi kwa washindi wa michuano hiyo Afisa Tarafa wa Somangila Ndugu Loyce Mwasaga amewashauri Wananchi kushiriki katika michezo mbalimbali ili kuimarisha Afya zao.

Aidha aliwataka kutumia michezo kama njia moja wapo ya kuimarisha ushirikiano pamoja na kuimarisha Muungano ulioasisiwa na Viongozi mbalimbali wa Taifa la Tanzania.

Katika Michuano hiyo zawadi mblimbali zilitolewa ikiwemo fedha Taslim, Mipira pamoja na





Baadhi ya wachezaji wa

# ZOEZI LA UPANDAJI WA MITI





**Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigamboni Bi. Pendo Mahalu akiongoza zoezi la upandaji wa Miti Kiwilaya**

Katika Kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Mhe Samia Suluhu Hassan la kuzitaka Wilaya zote Nchini kuhakikisha zinapanda Miti ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi.

Katika kuelekea maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wilaya ya Kigamboni iliendesha zoezi la upandaji wa miti lililofanyika katika viwanja vya shule ya Msingi mwongozo iliyopo katika kata ya somangila WIlayani humo ambpo jumla ya Miti 500 iliweza kupandwa.



**Katibu Tawala wa Wilaya akiongea na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwongozo**

Akizungumza na Wanafunzi wa shule hiyo katibu tawala huyo aliwa-taka kuwa na utamaduni

Aidh alitumia fursa hiyo kuwataka wana-funzi hao kuwa mabalozi kwa kutoa elimu ya umuhimu wa kupanda mitiwa kupanda miti ili kuepukana na hewa ya Ukaa.

# USAFI WA MAZINGIRA

Katika kuelekea Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Wilaya ya kigamboni iliendesha zoezi la usafi katika kata ya Kigamboni.

Lengo la kuendesha zoezi hilo ni kuhakikisha Wilaya hiyo inakuwa safi na inaepuka magonjwa ya mlipuko yanayoweza kuibuka kutokana na mrundikano wa taka Ngumu.

Aidha Wilaya iliweza kushirikiana na Uongozi wa Kata pamoja Serikali ya Mtaa wa ferry ili kufanya usafi katika eneo la Tanavamba.

Akiongoza zoezi hilo kwa niaba ya Mkuu wa wilaya ya Kigamboni Katibu Tawala wa Wilaya Hiyo Bi. Pendo Mahalu aliutaka uongozi wa Serikali ya Mtaa huo kushirkiana na wataalamu wa Idara ya Afya ili kutoa elimu kwa Wananchi ya namna ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Aliwataka watendaji hao kuacha tabia ya kukaa Ofisini na kusimamia usafi katika maeneo yao kwa kuanzisha kampeni mbalimbali za usafi katika maeneo yao.



Watumishi wa Manispaa ya kigamboni wakishiriki usafi



Wananchi wa Kata ya ferry wakishiriki katika zoezi la usafi Katani hapo




Zoezi la uzibuaji wa mitaro likiendelea katika Kata ya Ferry

## MIAKA 60 YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA: TUMESHIKAMANA NA TUMAENDELEO YA TAIFA LETUMEIMARIKA KWA

### HABARI KATIKA PICHA







**Manispaa ya Kigamboni inamshukuru Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuleta fedha kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekta mbalimbali**

**‘KAZI IENDELEE”….**










| | |
|---|---|
| **Limeandaliwa na** | **Mtayarishaji** |
| **Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni** | **Joseph Semkiwa** |
| **SLP 36009** | **Mhariri** |
| **Dar es Salaam** | **Honorata Minde** |
| **Chini ya** | **Mpiga picha** |
| **Kitengo cha mawasiliano Serikalini** | **Kinji Mwandika** |